

# VIPENGELE VYA UKARIMU WA MUNGU

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Katika makala hii mwandishi anavuta mawazo yetu kwa baadhi ya njia ambazo tunaweza kutambua ukarimu wa Mungu.

**Aina:** [Makala Imani za Uislamu Kuhusu Mwenyezi Mungu](#)

**Na:** islamtoday.net [edited by IslamReligion.com]

**Iliyochapishwa mnamo:** 08 Dec 2021

**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021

Mungu anasema:

***"Ewe mwanaadamu! Nini kilicho kughuri ukamwacha Mola wako Mlezi Mtukufu? Aliye kuumba, aka kuweka sawa, aka kunyoosha! Katika sura yoyote aliyo ipenda akakujenga."(Kurani 82:6-8)***



Swali katika aya hii ni balagha. Maana yake ni: "Je, hupaswi kumshukuru Mungu na kusifu sifa zake kwa baraka hizi?"

***Nabii Sulaiman (amani iwe juu yake) akasema: Haya ni katika fadhila zake Mola wangu Mlezi, ili anjaribu nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru, kwa hakika, anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anaye kufuru, kwa hakika Mola wangu Mlezi ni Mkwasi na Karimu." (Kurani 27:40)***

Jina la Mungu al-Karim Karim lina maana nyingi, kati ya hizo ni hizi zifuatazo:

## 1. Mwenye kutoa na Mwenye fadhila kubwa

Vivyo hivyo binadamu anaelezwa kuwa mkarimu ikiwa anawapa wengine kwa hiari na kwa moyo mkunjufu. Mtume Muhammad, rehema na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikuwa kielelezo cha ukarimu wa kibinadamu, kama walivyokuwa Mitume wote.

Mtume Muhammad aliwahi kuulizwa: **"Ni nani aliyekuwa mkarimu kuliko watu wote?"**

***Akajibu: "Mtu mkarimu ambaye alikuwa mwana wa mtu mkarimu, ambaye naye alikuwa mwana wa mtu mkarimu, ambaye tena alikuwa mwana wa mtu mkarimu:"***

***Yusufu mwana wa Yakobo, mwana wa Isaka, mwana wa Ibrahimu.*** [\[1\]](#)

Mungu ni mkarimu, anatoa bila kipimo kwa waja wake. Alitupatia uhai, ingawa hapo awali hatukuwepo. Alitupa uwezo wetu wa kusikia na kuona, mioyo na viungo vyetu, nguvu na uwezo wetu. Kweli: **"Kama mngehesabu neema za Mwenyezi Mungu, msingeweza kupata idadi."**(Kurani 16:34)

Anatupatia haya yote bila sisi kuomba wala kushukuru. Hakika, kwa kawaida hata hatutambui kwamba tumepewa chochote. Ukarimu wa Mungu unawajumuisha wale wanaomwamini pamoja na wale wanaokana Kuwepo kwake. Inamkumbatia mtakatifu na mtenda dhambi, mwenye elimu na mjinga.

## **2. Mwenye Kutoa na Kusifu**

Mungu pekee ndiye mkamilifu. Yeye pia ni mkamilifu katika kujitegemea Kwake, ambapo viumbe vyote vinamtegemea Yeye. Kila chembe ya mwili wa mwanadamu inamhitaji Mungu kwa uwepo wake. Licha ya hayo yote, Mungu hatoi tu kwa waja wake, bali ana wasifu na kuwasemea vyema.

***Kwa mfano, Mungu anasema kuhusu Ayubu (amani iwe juu yake):"Hakika tulimkuta mwenye subira, mbora wa waja, kwa hakika alikuwa mwingi wa kutubu." (Kurani 38:44)***

Baada ya kumjaribu Nabii Ayubu (amani iwe juu yake) kwa kumnyang'anya baadhi ya kile alichokuwa amempa hapo awali, anamsifu Nabii Ayubu kwa subira na uthabiti wake, ingawa chochote ambacho Mungu hutoa na kuzuilia ni cha Mungu tu kuanzia. Hata hivyo, mateso ya Nabii Ayubu yalipoisha, Mungu alimrudishia kile alichokuwa akikifurahia hapo awali cha baraka Zake, na akamsifu.

Mmoja wa Watangulizi Wacha Mungu aliposoma aya hii, alisukumwa na kusema: "Atukuzwe Mwenyezi Mungu ambaye huwapa na kuwasifu wale anaowapa."

Kadhalika, tunasoma katika Kurani ambapo Mwenyezi Mungu anawasifu manabii wake na watu wengine wema, akiwataja kuwa ni waamini, wamchao Mungu, wenye subira, wanao tubu na wasafi. Ni dhihirisho la ukarimu wa kweli sio tu kuwapa wale wanaohitaji, lakini kuwapongeza na kuwasifu sana.

***Mwenyezi Mungu alimwambia Nabii Sulaiman (amani iwe juu yake) baada ya kumpa ufalme tofauti na mwingine yeyote:"Hichi ndicho kipawa chetu. Basi toa au zuia, bila ya hisabu." (Kurani 38:39)***

## **3. Mwenye Kutoa Kabla Ya Kuombwa**

Ni ukarimu wa kweli kutoa bila kuombwa. Hakika sisi tunamwona mtu kuwa mkarimu ambaye hutoa kwa hiari kwa wale wanaoomba. Kufanya hivyo kabla ni ukarimu zaidi.

Baraka nyingi ambazo Mungu huwapa waja wake hutolewa bila kuombwa kamwe, au bila sisi hata kufahamu ni kiasi gani tunapewa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkarimu, Mwenye fadhila kubwa.

## **4. Anayetimiza Ahadi zote lakini Anakataza Yale Yanayostahili kutoka kwa Wengine**

Mwenyezi Mungu amewaahidi Waumini mema duniani na Akhera zawadi kubwa. Kamwe Mungu havunji ahadi yake. Wakati huo huo, Mungu amewaonya wale wanaofanya dhambi juu ya adhabu yake kubwa, kwa wale wanaostahili kwa kufanya dhambi na uovu. Hata hivyo, Amelifanya hili kuwa ni jambo la hiari Yake. Atawaadhibu wale wakosefu Anaochagua kuwaadhibu na kuwasamehe wale Anaochaguakuwasamehe.

Binadamu mkarimu ni mtu ambaye siku zote hutimiza ahadi kwa jambo zuri, lakini hatekelezi kwa vitisho. Ukarimu wa Mwenyezi Mungu ni mkubwa zaidi kuliko ukarimu wowote wa wanadamu tunaoweza kuufikiria, na Yeye ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.

## **5. Ambaye Kamwe Hamkatai Muombaji**

*Mtume Muhammad alisema: "Mola wako ni mwenye Unyenyekevu na ni Mkarimu. Mja wake anapo mnyooshea mikono, anaona aibu kumuacha mja huyo bila chochote."*<sup>[2]</sup>

*Mungu huwapa thawabu waja wake kwa kitendo chao cha kumuomba. Hii ni kwa sababu kumwomba kwetu Mungu ni kwa ibada. Hakika Mtume Muhammad amesema: "Dua ni ibada."*<sup>[3]</sup>

Kwa hivyo, Mungu huwajibu wale wanaomwomba kwa unyenyekevu.

## **6. Mtu Anayetuzia Nia Njema Tu, Lakini Haadhibu Nia Mbaya Isipokuwa Ikifuatwa na Tendo Mbaya.**

Mtume Muhammad alisema:

*Mwenyezi Mungu amebainisha mema na maovu na akabainisha (kwa waja wake) ni zipi. Basi anayekusudia kufanya jambo jema lakini halitendi, basi Mwenyezi Mungu ataliandika kuwa ni jema moja kamili katika kitabu chake.*

*Ikiwa atakusudia kuifanya na kuifuata, Mungu ataliandika kwenye kitabu chake kama kitu kutoka mara kumi hadi mia saba ya thamani ya tendo hilo.*

***Iwapo atakusudia kufanya tendo ovu lakini halitendi, Mwenyezi Mungu ataliandika kuwa ni tendo moja la kheri kamili lililorekodiwa kwenye kitabu chake.***

***Akitaka kulifanya na akalifuata, basi Mwenyezi Mungu ataandika kosa moja tu la uovu kwenye hesabu yake."***[\[4\]](#)

***Hatimaye, ni kutokana na ukarimu wa Mwenyezi Mungu kwamba Anawaheshimu watu katika dunia na Akhera, na akaufanya ucha mungu wetu kuwa ni sababu ya heshima. Mungu anasema: "Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi," (Kurani 49:13)***

Ni Mungu anayetubariki kwa ufahamu wetu wa Mungu na ucha mungu. Hii pia ni kutokana na ukarimu Wake mkubwa.

---

Rejeleo ya maelezo:

[1]

Saheeh Al-Bukhari, Saheeh Muslim

[2]

Sunan al-Tirmidhi, Sunan Abi Dawud, Sunan Ibn Majah

[3]

Sunan al-Tirmidhi, Sunan Abi Dawud, Sunan Ibn Majah, Sunan al-Nasai al-Kubra

[4]

Saheeh Al-Bukhari, Saheeh Muslim

Anwani ya wavuti ya makala hii:

<https://www.islamreligion.com/sw/articles/10704/vipengele-vya-ukarimu-wa-mungu>

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2023 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.